TANGAZO LA SERIKALI NA. 711 la tarehe 02/12/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA MEMBE YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Membe ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mpango wa jumla na wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

“Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MB1 yenye majira - nukta 182882E, 9354493N; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa $96.56^0$ kwa umbali wa kilomita 12.395 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba MB2 yenye majira - nukta 195196E, 9353076N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $153.827^0$ kwa umbali wa kilomita 7.318 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba MB3 yenye majira - nukta 198424E, 9346508N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa $196.974^0$ kwa umbali wa kilomita 8.036 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba MB4 yenye majira - nukta 196078E, 9338822N; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi na kukatisha na barabara ya Chilonwa -

*Tangazo la Serikali na. 711 (linaendelea)*

Dabalo katika uelekeo wa $274.836^0$ kwa umbali wa kilomita 11.375 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba MB5 yenye majira - nukta 184743E, 9339781N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa $328.827^0$ kwa umbali wa kilomita 11.335 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba MB6 yenye majira - nukta 178876E, 9349479N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki na kukatisha na barabara ya Chilonwa - Dabalo katika uelekeo wa $38.624^0$ kwa umbali wa kilomita 6.418 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*